

kikundi cha umri

10-15



Ndoa za

Utotooni



Ndoa za Utotoni ni nini?

Ndoa za utotoni ni pale msichana au mvulana wanapoingia katika ndoa wakiwa chini ya umri wa miaka 18. Kwa kawaida, ndoa hiyo huwa kati ya msichana na mwanaumwe aliyemzidi umri. Yaweza pia kuwa ndoa kati ya msichana na mvulana.

Kwa nini hili hutokea?

Zipo sababu nyingi zinazopelekea baadhi ya wanaume wenye umri mkubwa kutaka kuoja wasichana. Mara nyingi ni juu ya mila na tamaduni, na mawazo ya kizamani juu ya wanawake na wanaume.

Wakati mwingine, wasichana huolewa kwa kuwa wamepata mimba, au kwa sababu ya shinikizo kutoka kwenye familia kuwataka waolewe kabla hawajapata mimba. Wazazi pia wanaweza kuweka shinikizo kwa vijana kuingia katika ndoa kutokana na mila, au kwa vile wao ni maskini.

Je kuna ubaya gani katika Ndoa za Utotoni?

Ndoa za Utotoni huathiri afya ya msichana, elimu, Usalama, na furaha. Wasichana waolewapo wakiwa chini ya umri, ina maana:

- ▲ **Wasichana huacha kwenda shule.** Bila elimu nzuri, wasichana hawawezi kupata kazi nzuri itakayomuwezesha kuendesha maisha
- ▲ **Wasichana hupata mimba wakiwa katika umri mdogo,** kabla miili yao kuwa tayari. Hii huongeza hatari, na matatizo ya hatari, maradhi na hata kifo

- ▲ **Wasichana wapo katika hataari zaidi ya kupata VVU** na magojwa yatokanayo na ngono kwa kuwa hawajajengeka kikamilifu
- ▲ **Wasichana wana hatatari ya kufanyiwa ukatili kihisia, na kimaumbile.** Kutokana na nguvu za kimahusiano zisizolingana kati ya msichana na mwanaume
- ▲ **Wasichana hujikuta wamekatwa/wametengwa toka kwenye familia zao,** na marafiki zao ambao wapo bado shuleni

Wasichana wanaoolewa katika umri mdogo, hawako huru kufanya maamuzi yao wenyewe, wana majukumu mengi katika umri mdogo ikiwemo kuwa mama, kutekeleza majukumu ya nyumbani na kuwahudumia waume zao, pia hawana mda wala uhuru wa kujiangalia wao wenyewe au kupanga mambo ya baadaye.

Kuepuka ndoa za utotoni ni hadi pale ambapo msichana atakua tayari, hii inamaanisha kwamba msichana kuweza kufanya maamuzi yeye mwenyewe kuhusu maisha yake.

TUNAWEZAJE KUTOKOMEZA NDOA ZA UTOTONI ?

Hakuna njia rahisi ya kutokomeza ndoa za utotoni. Watu wazima na vijana ni lazima tufanye kazi kwa pamoja.

Wewe na marafiki zako mnaweza kuleta mabadiliko kwa kuwasaidia watu wazima kubadili mtazamo wa jamii jinsi wanavyochukulia ndoa za utotoni. Kuna njia mbalimbali za kufanya haya kama vile:

- ✓ **Kupaaza sauti** Katika jamii yako dhidi ya Ndoa za Utotoni.

Endapo wasichana watabaki mashuleni, basi huenda wakaolewa baadaye, wakawa na afya njema na salama na kupata fedha, hii itakua ni vizuri kwa wasichana kwa familia jamii na kila mmoja wetu.

- ✔ **Kuelewa** kuwa wasichana wanayo haki ya kufanya maamuzi yao katika maisha kama ilivyo kwa wanaume na wavulana wasichana wanaweza kuchagua waolewe na nani na wakati gani. Wanayohaki ya kuamua idadi ya watoto atakaotaka kuzaa. Wasichana pia wanayo haki ya ngono salama, kutumia kondomu na kujikinga na magojwa ya ngono ikiwa ni pamoja na VVU.
- ✔ **Kuwaeleza waalimu**, wazazi na viongozi katika jamii andapo utaona msichana analazimishwa kuolewa.

Watu wazima ambao wanataka kutokomeza ndoa za utotoni, wameweza kubadili sheria sehemu nyingi, na kulifanya suala la ndoa za utotoni kuwa ni kosa la jinai. Wanashirikiana na vijana kuhakikisha kuwa sauti za wasichana na wavulana zinasikika pale maamuzi muhimu yanapofanyika, kama vile kubadilisha sheria na sera.